## Mapendekezo

1. Sheria ya uvuvi haitakikani kulikimbiza kwa pamoja aina mbalimbali za uvuvi na mazuio yake. Kwa sababu ya tofauti za mfumo wa ikolojia na aina ya uvunaji rasilimali. Sheria ya uvuvi lazima itambue tofauti hizi.

2. Sisi hatuhusishwi na hatushirikishwi sana katika mipango na harakati za uundaji wa sera. Njia za kuwasilisha maoni na matatizo yetu ni chache na duni. Tunaomba wavuvi wajumuishwe vilivyo kwa uundaji wa sera kupitia mitandao ya wavuvi ya mashinani na ya kitaifa. “Kenya Marine Forum” inaweza pia kutuwakilisha.

3. Maeneo ya kinga ya ufuoni yamevamiwa na wastawishaji wa kibinafsi kutokana na unyonge wa kudhibiti sheria na ukosefu wa utiifu. Tunahitaji kuwa wakali mno juu ya udhibiti na utiifu wa sheria.

4. Hakuna nyaraka au hati ya utafiti inayothibitisha uwiano na uhusiano kati ya sheria bora, usimamizi endelevu wa uvuvi na manufaa ya kiuchumi na jamii. Hivi basi tunaona vigumu kupata motisha. Tugependa utafiti ufanywe kwa jambo hili ili tuone kinagaubaga uhusiano uliopo kati ya sheria na usimamizi bora wa uvuvi na kuboresha masilahi na uchumi wa jamii pamoja na upunguzaji wa umaskini.



Ofisi ya IUCN (muungano wa uhifadhi duniani) ya afrika mashariki na kusini, pamoja na CORDIO (shirika la utafiti na maendeleo ya pwani na bahari ya hindi) na EAWLS(shirika la afrika mashariki la viumbe hai porini) ziliandaa warsha mbili za jamii mwaka 2007/2008 nchini Kenya na Tanzania. Wakilishi wa jamii waliakisi na kuelezea hadhi ya mazingira ya bahari na kutoa mapendekezo thabiti ya kufanikisha rasilimali za bahari na uendelevu wa chuma riziki. Uchapishaji wa brosha hizi ni matokeo ya kazi hiyo.

Warsha za jamii ni sehemu mojawapo ya mradi mkubwa “uhifadhi kiini cha mali kwa chuma riziki katika afrika mashariki” unaofadhiliwa na IDRC (kituo cha kimataifa cha utafiti na maendeleo) na Ford Foundation. Pia mradi wa kujenga uwezo na kuimarisha sera za kuwaezesha jamii ya pwani kusimamia rasilimali zao za bahari katika afrika mashariki unaofadhiliwa na KNCF (mfuko wa fedha wa Kiedanren wa kuhifadhi viumbe). Madhumuni ya miradi hii ni kuongeza maarifa na ufahamu juu ya uhifadhi wa bioanuai unavyochangia chuma riziki na kuwasaidia jamii kudhihirisha umuhimu huu kwa wanasiasa na waundaji sera.

Maoni yaliyotolewa kwa chapisho hili si lazima kuwa mawazo ya mitizamo ya IUCN, IDRC,The Ford Foundation, KNCF, CORDIO au EAWLS.

Sifa kwa picha: Melita Samoilys/CORDIO
P. Harrison/Kilimanyika

IUCN IDRC CRDI

KNCF CORDIO East Africa THE EAST AFRICAN WILD LIFE SOCIETY

# Kujenga Uwezo wa Jamii Kusimamia Rasilimali ya Baharini Kenya



# Wavuvi wa Pwani Kenya

Na:
Salim Ali Hiribae
Abdalla Jillo
Hamisi Hamadi
Shaibu Mohamed

## Utangulizi

Uvuvi wa Kenya aghalabu huwa wa maji baridi ya maziwa na maji ya chumvi ya bahari. Sekta ya uvuvi ni muhimu katika itkisadi na ustawi wa uchumi na maendeleo ya humu nchini na hutoa riziki kwa zaidi ya wakenya 600,000. Eneo la bahari limejaliwa na rasilimali tele za uvuvi. Lakini, uvuvi wa baharini huchangia chini ya 5% ya uzalishaji wa kitaifa wa samaki. 95% ya uzalishaji wa samaki hutoka maji ya bara hasa ziwa Victoria.

Wavuvi wengi wa pwani ni wadogo wadogo na uvuvi wao ni wa kijungujiko. Uvuvi mwingi hutawaliwa na kufanywa na wanaume. Uvuvi mwingi hufanyika bahari ya karibu, maji ya kina kifupi na miambani. Ni nadra uvuvi kutekelezwa nje ya maji ya taifa. Uvuvi mwingi hutekelezwa kwa kutumia matumbwi. Zana zinazotumiwa kwa wingi ni nyavu za juya, mitego na mishipi.

Mazao makuu ya uvuvi ni pamoja na, jodari, kamba, kambakoche, pweza na ngisi. Kwa jumla kila mahali kuna upungufu wa mazao na mashiko ya samaki.
Uhaba wa kutumia na usimamizi duni wa uvuvi wa pwani na baharini umesababishwa na yafuatayo.

Upungufu wa bandari za kutua samaki. Wavuvi wengi huwa na shida ya kuingia na kutumia bandari hizi kutokana na ujenzi wa mahoteli, nyumba za watu binafsi na miradi holela mingine.

Ukosefu wa mikopo, miundo misingi na utaalamu. Hasara ni kubwa mno baada ya mavuno na gharama za uzalishaji na uuzaji ni za juu kwa wavuvi wa kawaida.

Wavuvi hawana mashirika dhabiti ya kuwawakilisha. Hivyo, hawajawakilishwa ipasavyo katika kongamano za kitaifa za maamuzi na ushawishi wa sera za serikali.

Idara ya uvuvi ambayo chini ya sheria ya uvuvi (sura 378) ina jukumu la kusimamia rasilimali za uvuvi nchini, haina vifaa muhimu kuiwezesha kutekeleza barabara kazi yake. Ina ukosefu wa vifaa vya kupigia doria, vifaa vya mawasiliano na mashua.

Inapunguza juhudi za kudhibiti uangalizi. Matokeo yake ni uvuvi usio na utaratibu, uvuvi haramu na usioratibiwa na kuripotiwa katika bahari ya Kenya unaofanywa na wavuvi wa kigeni.

Warsha ya kitaifa ya jamii ya pwani ilifanyika Kilifi kuanzia tarehe 17 hadi 19 Desemba 2008. Lengo la warsha lilikuwa kuzipa jamii za pwani fursa ya kutangamana na kubadilishana uzoefu wa usimamizi na utendaji kwenye rasilimali za baharini pamoja na kuelezea kwa ufasaha mahitaji yao. Kama wakilishi wa wavuvi wa pwani, tulitoa maoni yetu, malengo, shughuli, masuala nyeti na mapendekezo katika mkutano huo.

## Maswala nyeti

Maeneo ya kitaifa ya uvuvi wa Kenya yanazidi kutumiwa na kuvuliwa kupita kiasi. Hii inasababishwa na ongezeko la wavuvi wa humu nchini na wale wa kigeni wanaovamia na kushinikiza ralisimali. Kwa mfano, Wapemba kutoka Tanzania wanavua katika mwambao wote wa Kenya kuanzia Vanga-Shimoni hadi Kipini na Lamu. Kenya haijawadhibiti wavamizi hawa hasa kuhusiana na kutathmini uvuvi wao.

Uvuvi wa kutumia jahazi za bahari ya kina umeongezeka. Ingawa leseni zinatolewa kwa jahazi hizi, kuna upungufu wa ufuatilizi wa uvuvi na uchunguzi wa leseni zao. Hivyo wenye leseni hupuuza masharti ya leseni hizo na kuvamia maeneo ya wavuvi wadogo wadogo.

Matokeo ya matatizo haya yote ya uvuvi ni upungufu wa mazalio na mazao ya samaki, kushuka kwa pato la samaki na kuangamia kwa aina fulani ya samaki wanaovuliwa.

## Usimamizi wa uvuvi wa pwani nchini Kenya

1. Sheria inayotumika sasa ya uvuvi imeweka taratibu ya aina moja tu juu ya zana zinazotumika katika uvuvi na maeneo yote ya bahari. Lakini usimamizi na taratibu unatakikana kuwa tofauti kulingana na tofauti ya mastakimu na aina ya samaki. Ingekuwa bora kama usimamizi ungechanganua rasilimali ya uvuvi kulingana na tofauti za kiikolojia na zana muafaka kwa kila aina ya samaki. Kwa mfano nyavu haziwezi kutumiwa kuvuilia dagaa na kiboma kwa wakati mmoja.

2. Matumizi kiholela ya zana halali na vifaa haramu vinachangia uharibifu wa mazingira ya bahari na samaki. Mifano ya mbinu haribifu ni matumizi ya baruti na sumu. Ingawaje matumizi ya jarife na 'ringnet' yanakubalika kutumika kwa maji ya kina kirefu, haitakikani kutumika kwenye miamba au maji ya kina kifupi kwani itaharibu.

3. Matumizi ya njia haribifu na haramu mathalani huchungiwa na ukosefu wa hasama na ujuzi wa kutoarifiwa juu ya sheria zinazodhibite tasnia ya uvuvi miongoni mwa wavuvi. Hali kadhalika kuna uhaba na unyonge wa kutathmini, kuchunguza na kukagua kuhakikisha taratibu zinazingatiwa na wavuvi wote.

4. Watu bado hawajatambua au kukubali umuhimu wa uvuvi wa bahari katika kuchangia kwa ustawishaji wa maisha na masilahi ya jamii ya pwani na uchumi wao.



## Muhtasari wa malengo, shughuli na maswala husika ya kijamii

| SHIRIKA/KIKUNDI | MALENGO NA SHUGHULI | MASWALA HUSIKA |
|---|---|---|
| Chama cha ushirika cha wavuvi wa Mwagugu Vanga-Kwale | • Kupata soko la samaki waliovuliwa<br>• Kutoa mikopo kwa wanachama wa shirika<br>• Kuondoa umaskini<br>• Kutoa vifaa vya kuhifadhia samaki kwa wanachama | • Ukosefu wa ujuzi wa usimamizi<br>• Kushuka kwa pato la samaki pamoja na tofauti za samaki |
| Wavuvi wa Kilelenjwani | • Uvuvi | • Ukosefu wa zana bora za uvuvi |